

# HALMASHAURI YA WILAYA YA KIGOMA

(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji Wilaya)

Tel. 028280 4865

Fax. 028280 2719/2370

Email: [Ded@Kigomadc.Go.Tz](mailto:Ded@Kigomadc.Go.Tz)



Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji,  
S.L.P. 332,  
Kigoma.

Kumb.Na.KDC/S1/2/77

Tarehe: 01 Novemba, 2021

## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma anapenda kuwatangazia watananzania wote kuwa ofisi imepokea kibali cha Ajira Mbadala kutoka kwa Katibu Mkuu UTUMISHI chenyé Kumb.Na.FA.170/358/01"C"/66 cha tarehe 13.09.2021 kwa ajili ya kutangaza nafasi ya kazi ya Mtendaji wa Kijiji III kwa masharti ya kudumu. Hivyo Watanzania wote wenye sifa mnaombwa kuomba nafasi hiyo kama ifuatavyo:

### 1. MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA LA III (VILLAGE EXECUTIVE III) - NAFASI NNE 4).

#### i. Sifa za kitaaluma kwa Mwombaji

Kuajiliwa mwenye kidato cha Nne (IV) au sita (VI) waliopata mafunzo katika ngazi ya cheti (NTA LEVEL 5) ambao wamehitimu Mafunzo ya Astastahada / Cheti katika moja ya fani zifuatazo:

- Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka Katika Chuo cha Selikari za Mitaa Hombolo Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

#### ii. Majukumu ya kufanya:

- a. Afisa Masuhuli na Mtendaji mkuu wa Serikali ya Kijiji.
- b. Kusimamia ulinzi na Usalama wa Raia na mali zao, kuwa Mlinzi wa Amani na msimamizi wa Utawala Bora katika kijiji.
- c. Kuratibu na kusimamia upangaji na utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya kijiji.
- d. Katibu wa mikutano wa kamati zote za Halmashauri ya Kijiji.
- e. Kutafsiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu.
- f. Kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, Umaskini, nakuongeza uzalishaji mali.
- g. Kiongozi wa Wakuu wa Vitengo vya kitaaluma katika Kijiji
- h. Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za Kijiji.
- i. Mwenyekiti wa kikao cha Wataalamu waliopo katika kijiji.
- j. Kupokea, kusikiliza na kutatua malalamiko ya Wananchi
- k. Kusimamia utungaji wa sheria ndogo za Kijiji na
- l. Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata.

**III. Masharti ya Ajira:**  
Ajira ya kudumu

**iv. Ngazi ya Mshahara:**  
Ngazi ya Mshahara ni kuanzia ni TGB B

*Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 15/11/2021 saa tisa na nusu (09:30) Alasiri*

Maombi yote yatumwe kwa

**MKURUGENZI MTENDAJI (W),**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KIGOMA,**  
**S.L.P 332,**  
**KIGOMA**

Tangazo hili limetolewa na:

Rose R. Manumba  
**MKURUGENZI MTENDAJI**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KIGOMA**

*MKURUGENZI MTENDAJI  
HALMASHAURI YA WILAYA  
KIGOMA*